

## **USIMAMIAJI WA KANUNI ZA MAADILI YA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA.**

### ***Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma***

#### **1.0 Utangulizi**

Katika makala ya wiki iliyopita tulieleza namna ambavyo serikali inashughulikia mafao ya watumishi serikalini. Katika makala hiyo tulielezea kuwa mafao ni malipo anayopata mtumishi baada ya kustaafu kazi katika utumishi wa umma. Aidha tuliezea pia kuwa mamlaka za zinazohusika na utayarishaji wa kumbukumbu za mtumishi zinapaswa kutunza na kuziwasilisha kumbukumbu hizo kwenye Mifuko husika ili Mifuko iweze kuandaa mafao ya mtumishi husika kwa wakati. Katika makala ya leo tutaelezea usimamiaji wa kanuni za maadili ya kazi katika utumishi wa umma. Sote tunajua kuwa utendaji wa shughuli za serikali huongozwa na kanuni za maadili ya kazi zilizotolewa na serikali kwa ajili ya watumishi wote wa umma. Watumishi wote wa umma wanao wajibu wa kufanya kazi kwa kufuata kanuni za maadili ya kazi. Aidha mamlaka za nidhamu zinapaswa kusimamia utekelezaji wa kanuni za maadili ya kazi katika utumishi wa umma kwa kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinafuatwa na kila mtumishi ili kujenga nidhamu ya utendaji wa shughuli za serikali kwa kuwaelimisha na kutoa miongozi muhimu kwa watumishi wote wa umma.

#### **2.0 Utekelezaji wa kanuni za maadili ya kazi katika utumishi wa umma**

Ili watumishi wa umma waweze kutekeleza shughuli zao kwa kufuata kanuni za maadili ya kazi mamlaka za nidhamu katika utumishi wa umma zina wajibu wa kutekeleza yafuatayo:

2.1 Kuwapatia watumishi mwongozo wa kanuni za maadili ya kazi katika utumishi wa umma (Kanuni Na.66(1). Katika hatua hii mamlaka za nidhamu zinapaswa kuhakikisha kuwa kila mtumishi amepatiwa nakala ya mwongozo wa kanuni za

maadili ya kazi ili kila mmoja aweze kusoma na kuelewa yale ambayo yameelekezwa katika mwongozo huo.

2.2 Kumsainisha kila mtumishi makubaliano ya kuzingatia kanuni za maadili ya kazi katika utumishi wa umma(kanuni Na.66 (2) kwa kutumia fomu za makubaliano ya kuzingatia kanuni za maadili ya kazi. Fomu hii itajazwa na mtumishi na kuthibitishwa na mwajiri

2.3 Kuchukua hatua dhidi ya mtumishi anayekiuka kanuni za maadili ya kazi(kanuni Na.67). Katika kutekeleza hatua hii mamlaka za nidhamu zinapaswa kutekeleza hatua hii kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na sheria nyingine za nchi.

### **3.0 Hitimisho**

Mamlaka zote za nidhamu zinapaswa kutekeleza masuala yote ya kinidhamu kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa umma Na 8 ya mwaka 2002, kanuni na taratibu zake za mwaka 2003.

Ndugu msomaji, iwapo una maswali au maoni tafadhali tuandikie:

Katibu,

Ofisi ya Rais

Tume ya Utumishi wa Umma

Jengo la Acacia, Mtaa wa Samora

S.L.P 9143

Dar es Salaam.

Simu: +255(22) 2126811/4, 216260 Faksi: +255(22) 2114158